

VEDLEGG: VEILEDER TIL INTEGRERINGSPLAN

Maelezo kuhusu mpango wa ujumuishaji katika jamii kwako wewe utakayehudhuria katika introduksjonsprogram (Mpango wa masomo na utayarishwaji wa kujitegemea)

Mpango unaokuhusu wewe

- Manispaa yako unapoishi itashirikiana na wewe kutengeneza mipango ya jinsi utakavyoshirikishwa kupitia uhudhuriaji wako katika masomo yanayokutayarisha kwa kujifunza lugha na kujiandaa kuwa mfanyakazi. Uhudhuriaji wako katika introduksjonsprogram utachangia katika uwezekano wako wa kujua lugha ya ki Norwej, elimu ya jamii ya Norway, kufuzu masomo ya taaluma na mahusiano ya kudumu ya maisha ndani ya ajira. Lengo letu ni kukushirikisha mapema katika jamii ya Norway kusudi uwe na uwezo wa kujitegemea ki uchumi.

Ukusanyaji wa taarifa za ujuzi

- Kabla hujafanya mpango wa ujumuishwahi unapaswa na ni haki yako kufanya ukusanyaji wa taarifa zako za ujuzi wako. Taarifa zako zinapaswa angalau kuwa na maelezo ya ujuzi wako wa lugha, na kiwango cha elimu yako, ujuzi wa kazi, na aina nyingine za elimu kwa njia ya uzoefu wako.

Ushauri wa fani

- Una haki na wajibu wa kufanyiwa ushauri wa fani. Ushauri wa fani utakusaidia kukupatia maelezo yanayokuwezesha kufanya mipango yako ya elimu na aina ya kazi.

Yaliyomo katika mpango wa ujumuishaji

- Mpango wa ujumuishaji unapaswa kuwa na lengo la hitimisho na lugha ya kinorwej, mpango wa elimu, muda utakatumia kuwepo katika mpango huu, na pia nafasi uliyo nayo ya kukata rufaa ikiwa hukubaliani na mipango hii. Mipango yako itategemea taarifa zako za elimu yako, uzoefu wa kazi, ujuzi kulingana na kazi ulizofanya maishani mwako, na maelezo mengine ya ziada.

Mpango wa ujumuishaji utakuwa na angalau:

- a) Elimu ya lugha ya kinorwej
- b) Elimu ya jamii
- c) Kozi ya uwezeshwaji wa maisha
- d) Vipengele vya – Mafunzo ya kazi au mafunzo ya elimu

Wanafunzi wenye Watoto wa umri chini ya miaka 18 watapaswa kuingia katika kozi ya maelekezo ya malezi.

Mpango wa masomo utakuwa ni wa kudumu kwa mwaka mzima.

Uhitimu wako

- Manispaa itapanga uhitimu wako katika uhudhuriaji wako masomoni. Uhitimu wako utategemeana na kiwango cha elimu uliyo nayo tangu awali.

Lengo la kujifunza lugha

- Wanafunzi wa lugha ya kinorwej wanapaswa kufuzu kiwango cha chini cha lugha. Manispaa na mkoa watawajibika na kuhakikisha kwamba mwanafunzi anafuzu kiwango cha chini cha lugha.

Ufuatiliaji na upimaji wa mpango wako wa ujumuishwa.

- Wakati wa masomo yako, manispaa itatekeleza majadiliano ya jinsi ambavyo mpango wako wa ujumuishwaji unavyoendelea. Kama hufanyi kama ulivyokuwa umepanga, au kama hutaki mipango ile ya awali, inakupasa utoe taarifa haraka sana kwa kadri iwezekanavyo kwa kupitia kwa mshauri wako.

Ungependa kulalamikia mpango wako wa ujumuishwaji?

- Unaweza kutuma malalamiko yako juu ya elimu au yaliyomo katika mpango wako wa ujumuishwaji.

Ikiwa unataka kutuma malalamiko yako fanya yafuatayo:

- Peleka malalamiko yako kabla ya majuma matatu hayajapita tangu upatiwe maelezo yanayohusu mpango wa ujumuishwa.
- Peleka malalamiko yako kwa kitengo cha manispaa kilichotoa maamuzi unayolalamikia
- Andika unacholalamikia
- Lazima utie sahihi/saini yako

Unaweza kutuma malalamiko yako kupitia kwa muwakilishi wako. Muwakilishi wako atakubalika pale tu ambapo atakuwa na barua ya maandishi ya kuthibitishwa nawe. Barua ya uthibitisho ni lazima ioneshe kile ambacho muwakilishi wako anapaswa kukifanya kwa niaba yako wewe. Ikiwa una mwanasheria basi huhitaji kumpatia barua ya uthibitisho.

Maelezo zaidi kuhusu mpango wa ujumuishwaji yanapatikana wapi?

Maelezo zaidi kuhusu mpango wa ujumuishwaji waweza kuyapata katika sheria ya ujumuishwaji wa jamii. Sheria na kanuni zake inapatikana www.imdi.no na Kompetanse Norge nettsider.

Kila la kheri katika masomo yako!